Harvey, Andrew, Hezekiah Kodi, Josiah Sumaye, Raheli Lawi, Andrea Tsino, Paschal Bu'ú, Stephano Edward, and Festo Massani. 2016. Gorwaa Language Project: Action Plan I (2017-2022); Babati - August 2016 / Mradi wa Lugha ya Kigorowa: Mpango Kazi I (2017-2022); Babati - Agosti 2016 DOI: 10.5281/zenodo.2535899

# Mradi wa Lugha ya Kigorowa
# Mpango Kazi I
# 2017-2022

## Utangulizi

Mpango kazi ufuatao umekuja kama matokeo ya miaka mitano ya mahusiano ya karibu sana baina ya wajumbe wa Kamati ya Jamii ya Lugha ya Gorwaa (Josiah Sumaye, Hezekiah Kodi, Raheli Lawi, Andrea Tsino, Paschal Buu, Stephano Edward na Festo Massani, na Mtaalamu mtafiti wa kigeni wa Lugha Andrew Harvey). Mpango huu umekusudiwa kutumika kama wajibu kuakisi hali halisi ya upotevu wa lugha ya Gorowaa, pia kama njia kuelekea ufufuaji wa lugha na uboreshaji wake katika jamii.

## Kubainisha chanzo cha msingi wa sababu hatarishi ya lugha ya Gorwaa

Lugha ya ya Gorwaa ipo kwenye hali mbaya sana ya kudidimia, ikiwa na wanenaji au watumiaji fasaha wachache, na nafasi au wasaa adimu wa kutumia, katika zoezi lililoendeshwa ili kupata chanzo cha msingi wa sababu inayohatarisha lugha ya Gorwaa, mambo yafuatayo yaliyojitokeza;

Lugha ya kigorowa na tamaduni zinapotea

Hii kwa sehemu kubwa inatokana na:

*Lugha na mila ya asili ya Gorwaa kutokutumika.*

Mambo yanayochangia:

-makatazo(Kisheria na Kijamii) katika matumizi ya lugha na asili na matendo fulani ya kitamaduni.

-mabadiliko muhimu ya mazingira ya kienyeji (yote mawili-kijamii na kimazingira) yaliyotekwa na ukoloni, serikali ya taifa na utawazi.

-kudidimia kwa mapokeo ya mila mara kwa mara mategemeo ya maandishi ya sasa (hali Gorwaa ina ukosefu mkubwa wa mfumo unaojulikana wa maandishi (uandishi))

*Wazazi hawawapokezi watoto lugha na mila au utamaduni*

Mambo yanayochangia:

-Gorowa hakizungumzwi tena nyumbani.

-tamaduni za asili (mila) hazifanyiki tena nyumbani

-famila leo ni za mchanganyiko (katika ndoa)

-mfumo wa sasa wa maisha (hasa saa za kazi –muda mrefu wa kazi) na shuleni umechukua wajibu wa wazazi kama mwalimu na badala yake serikali ikachukua nafasi hiyo.

-vyanzo vya asili vya habari na burudani zimepigwa teke na habari za umma na jamii (zimechukuliwa)

*Kutokuwa na usawa wa jinsia*

Mambo yanayochangia:

-nafasi halisi ya uwezo wa mwanamke katika utamaduni wa jamii ya Gorwaa haijulikani sasa au haieleweki vizuri.

-wanawake siku hizi hawana muda wa kuweza kuendeleza lugha ya Gorwaa kwa sababu ya uzito wa kazi walizowekewa (kupika, kutunza watoto na mengineyo).

*Watu hawathamini tena lugha yao na utamaduni wao*

Mambo yanayochangia:

-watoto kufundishwa (moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja) kwamba lugha ya kigorwa ni mbaya.

-watu wa Gorwaa kukosa nafasi na matukio ambayo yanahusisha jamii na kutenda kama watu wa Gorwaa.

-hadithi au habari za kifamilia haziendelezwi

-elimu rika haiendelei kutolewa.

*Umaskini au ufukara uliokithiri pote huuweka ukarabati na maendeleo ya lugha nyuma kimahitaji*

-Kiingereza na Kiswahili vyote viwili hutambuliwa kama lugha za biashara na kujiendeleza (kujikimu) au kuendelea kama gharama za kufifisha lugha ya Gorwaa kama lugha isiyo na thamani

-kazi inayohusiana na ukarabati na maendeleo ya lugha haionekani kama yenye kuleta mapato (kama hailipi)

-mapato yasiyokidhi mahitaji ya msingi yanachangia upotevu wa lugha na mila (asili).

**<u>Ukarabati wa lugha ya Gorwaa: Maono</u>**

Kufuatia kutambuliwa kwa baadhi ya mazingira ya sababu zilizohatarisha lugha na mila ya Gorwaa, watu binafsi walipewa kubashiri dunia ambayo lugha au mila ya Gorwaa inavyokarabatiwa na kuendelezwa hivi ndivyo walivyosema

<u>Ndoto-Maoni</u>

*Ya watu*

-watu kujitoa wenyewe wakiwasaidia jirani zao.

-vijana wanapewa nafasi ya elimu rika

-vijana  kutambua na kuelewa thamani ya utamaduni

-wageni wanatiwa moyo na watu wa Gorwaa na kuhawahamasisha na kujenga jamii kwenye makusudio yao

-watu wana afya

-watu wanajivunia mavazi ya asili (ya utamaduni) na kuvaa mara kwa mara.

-nafasi ya kuwa pamoja kama watumia Kigorowa inapatikana, usawa wa jinsia ni uhalisia.

*Ya ardhi*

-mazingira yaliyoharibiwa yanajengwa upya ili kudumisha matazamio ya utamaduni.

-nchi(ardhi) ni ya kijani

-miti, mito, misitu na sehemu zenye maji inatumika

-mbolea za asili kuchukua nafasi ya kemikali za kisasa na matumizi ya madawa ya asili ya kuulia wadudu

-hakuna njaa tena.

*Ya kazi*

-'maendeleo' yanaendeshwa na watu wenyewe badala ya kuongozwa na serikali peke yake.

-matibabu ya asili ya kibayolojia yanaeleweka kama dawa na kutumika pindi yapatikanapo.

-nyimbo za asili kujulikana na kuimbwa

-michezo ya asili hujulikana na kuchezwa.

-watu hulima na kula mtama pamoja na vyakula vinginevyo vya asili.

-kazi za ushirikiano wa kimila au asili hufanyika (sehemu zote, shambani au penginepo)

-Kigorowa kinazungumzwa kazini, katika katika mikutano ya jamii, kanisani, nk. Watu wasiozungumza Kigorowa kuhakikishwa watafsiri(wakalimani)

-vijana kuajiriwa

-gharama za maisha kukidhiwa (kupatikana).

**Kuleta badiliko hatua maalum pendekezwa 2017-2022**

Pamoja na misingi ya sababu za matatizo ya leo yaliyotajwa pamoja na maono ya baadaye yenye ufanisi au uwezo, watu binafsi walianzisha orodha ndefu ya mapendekezo ya hatua ambazo zitachukuliwa katika miaka mitano ijayo. Kwa kufuata mfululizo ambao hatua pendekezwa zimetathminiwa kufuatana na jinsi zitakavyofanikisha kushughulikia misingi ya sababu husika na kusaidia kufikia maono, mambo yafuatayo yalionekana kama kipaumbele kwa 2017-2022.

Kuanzisha kamati ya kujitegemea:

Watu binafsi walielekeza kuwa mengi ya hatua zenye ufanisi ambazo zitaweza kuchambuliwa ili kukarabati na kuendeleza lugha ya Gorwaa na mila (utamaduni) zitachukuliwa na watu binafsi na makundi huru ya jamii (familia, klabu, vyama vya ushirika na kadhalika). K wa hayo yaliyosemwa bado inakubalika kwamba kuanzishwa kwa kamati ndogo maalumu ambayo jukumu lake kuu ni ukarabati na maendeleo ya lugha ya Gorwaa. Hii ni hatua muhimu ya kutambua nguvu ya maono yaliyotajwa hapo juu.

Kamati itafanya kazi kuelekea maono kwa:

1A. Kuchukua hatua katika mpango kazi huu kupitia maendeleo kila mwaka, kuendelea daima kutathmini ufanisi wa mpango kazi (na taarifa fanisi itakayochapishwa kila mwaka wa nne)

1B. Kuendeleza mpango kazi kwa miaka; 2022-2027 (Maendeleo kuanza si zaidi ya 2021)

1C. Kukutana kila baada ya miezi 3

1D. Kuwa na mikutano isiyo ya kawaida ambapo, na kama itahitajika.

Imekubalika kuwa ni muhimu sana kwa kamati ya kuwa ni ya kujitegemea. Hayo yaliamuliwa kuwa msaada kidogo uwe msingi wa uwekezaji wa jamii na hatimaye kuwa msingi wa mfuko unaokua wa kamati na hatua zake na hatua zake au mipango kazi yake.

Uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya Gorwaa nyumbani:

Matumizi ya lugha ya Gorwaa nyumbani kumetambuliwa kama hatua inayofanya kazi katika ukarabati na kuendeleza lugha na utamaduni wa Gorwaa. Hii ni hatua mchanganyiko na thabiti ya hatua zilizotajwa na itahitaji muafaka wa hatua ya muda mrefu itakayokamilishwa kwa ufanisi.

Hatua hii itahusika na;

2A. Kuhamasisha utafiti wa kielimu kwa:

1)Kutambua sababu za kwa nini lugha ya Gorwaa haiendelei kuzungumzwa nyumbani.

2) Kushauri kwa ustadi kuboresha matumizi yake nyumbani

2B. Kutenda katika mapendekezo yake ya ustadi.

2C. Kutathmini ufanisi wa maono yake.

Kuhamasisha lugha ya Kigorowa kwenye jamii:

Kutumia lugha ya Gorwaa katika jamii kubwa kumetambuliwa kama njia kuu ya kuinua mpango wa lugha na hatimaye kupanuliwa orodha ya maeneo ambayo lugha ya Gorwaa inazungumzwa. Huu ni mpango mrefu ambao hatimaye utafanikiwa katika mfululizo wa hatua ndogo ndogo zilizolengwa vizuri.

Hatua hii itahusika na:

3.A. Kutambua orodha za jamii ya Gorwaa ambako lugha ya Gorwaa inahamasishwa. Orodha hii inaweza kuhusisha:

-maeneo ya ibada(Sehemu zote mbili za imani ya kikristo nay a kiislamu).

-maeneo ya michezo - timu za michezo.

-vyama vya uwekezaji (vikoba) n.k.

-majirani-ujirani

3.B. Kuwa na mikutano midogo na wajumbe wa vikundi ili kutambua ustadi wa mtu binafsi kwa kutambulisha au kutumia lugha ya Gorwaa.

3.C. Kwa kufanikisha ustadi huu wa mtu binafsi kuhakikisha mafanikio yao na kuboresha kadiri inavyohitajika. Hatua hii lazima itekelezwe kwa ushirikiano na wajumbe wa vikundi vyenyewe.

3.D. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

Kuendeleza maombi ya mila hasa kwa kamati ya lugha ya Gorwaa:

Moja ya hatua za kwanza kujulishwa ni ile ya kujitoa (kujihusisha) kwenye kusudi (kujikabidhi). Kujikabidhi huku lazima kutoke kwenye wajumbe wa kamati, waandamizi, na watu mashuhuri katika jamii na waalikwa. Watu wa Gorwaa wana utamaduni tajiri wa maombi ambao bado unafanyika na wazee wa jadi(mila). Kuendeleza maombi ya mila kuthibitisha kujitoa kwa mtu kwa ukarabati na uendelezaji wa lugha na utamaduni wa Gorwaa itakuwa alama madhubuti pamoja na hatua fupi mahususi. Na rahisi.

Hatua hii itahusisha:

4.A. Kumtambua mzee au kikundi cha wazee ambao wanaweza kuendesha maombi(sala) ya Gorwaa.

4.B. Kuwaeleza kwa makini kusudi la maombi.

4.C. Kufanya kazi nao kuendeleza maombi ya kujitoa kwa muda mfupi.

4.D. Kuhakikisha kuwa maombi haya yanatumika katika mikutano ya kamati na matukio n.k.

4.E. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

Kufufua elimu rika (iliyokusudiwa):

Elimu rika ilitambuliwa kama mbinu mojawapo yenye ufanisi wa kuziba ufa (daraja) katika jamii kuinua umakini wa mila ya Gorwaa na historia yao na kuandaa nafasi kwa watu wa Gorwaa kuwa Wagorwaa.

Kwa hayo yaliyosemwa hatua hii ni ya hisia kali kimila ikiwa na mambo maarifa ya siri kufanya kazi na vijana na kubakia kweli kwenye mambo yahusuyo utamaduni vs kuendeleza vitendo vilivyojiri kushughulikia mambo muhimu kabla ya kurejeza utamaduni huu muhimu.

Hatua hii itahusika na:

5A. Kuhamasisha utafiti kieleimu kwa;

1. Kuelewa jinsi ya kujishughulisha na maarifa ya siri ya mila ya Grwaa.
2. Kuendeleza mafundisho –makakati unaofaa kufanya kazi na vijana.

3. Kutambua mbinu ya kujenga elimu rika mpya tofauti na ile ya zamani.

5B. Kuendeleza utafiti mkabila na watu binafsi ambao wamehusishwa katika elimu rika.

1. Kuelewa mambo yaliyomo kwenye elimu rika.
2. Kujenga mahusiano ya kuaminika kwa wanajamii husika.

5C. Kufanya kazi kwa karibu na watu binafsi ambao wamehusishwa katika elimu rika, kuendeleza na kuwekeza katika mradi mdogo kupima nini kilichofundishwa na kutathiminiwa, na kuboresha kadiri inavyoonekana muhimu.

5D. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

<u>Kuwa na maonyesho ya utamaduni na lugha ya Kigorowa:</u>

Kuwepo na makundi ya mila walioendeleza nyimbo za gorwaa, ngoma za kitamaduni, kuwa maonyesho makubwa kuweka lugha ya Gorwaa na mila katika kuweka wazi kwa kutambua kama hatua rahisi.
Kwa yasemwayo kwa kipimo hiki ni tukio la gharama kubwa.

Hatua hii itahusika na;

6A. Kutambua eneo la kufanyika kwa tukio hili pana.

6B. Kukutana na wawakilishi wa jamii, serikali, shule, makundi ya mila na nk. Kuandaa au kibuni tukio la kijamii.

6C. Kuendeleza makisio (bajeti) = makadirio.

6D. Kuwa na tukio, hakikisha unatunza mahudhurio. Kuandaa taarifa ya kina kuhusu matokeo, kuchukua picha.

6E. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

<u>Kuunda kumbukumbu za nyimbo za Gorwaa:</u>

Wimbo ni chombo chenye nguvu sana kwa kuinua utambulisho na uwezo wa kutumika kwa ufanisi zaidi kuanzisha utaratibu (kanuni) kote katika utamaduni wenyewe wa nyimbo za Gorwaa na pia katika lugha na mila kwa ujumla ; mradi huu ni wa kipimo cha kati hasa ulio ghali.

Hatua hii inahusika na;

7A. Utambuzi wa kumbukumbu za nyimbo-nyimbo 12 -15, unaeleza tofauti mbali mbali, uimara na asili kuu ya utamaduni wa nyimbo za Gorwaa.

7B. Amua jinsi kila wimbo unavyowekwa kwenye kumbukumbu (utakavyorekodiwa), uwekaji wa hali ya juu ya kumbukumbu, sauti na vikundi vidogo vidogo, nyenzo za vikundi vikubwa n.k.

7C. Kutambua na kuchagua watu binafsi kufanya na kurekodi kumbukumbu.

-Tambua kituo (studio) thabiti cha uwekaji wa kumbukumbu chenye uzoefu wa kutosha katika kurekodi nyimbo za asili (mila).

7D. Rekodi nyimbo(weka kwenye kumbukumbu)

7E. Anzisha kampeni ya kusambaza au kueneza nyimbo (bure au kwa faida).

7F. Anzisha soko-uenezaji wa nyimbo.

7G. Tathmini ufanisi wa hatua hii.

<u>Kuendeleza watafiti wenyeji:</u>

Miaka kadhaa ya kazi na mtaalamu wa lugha wa kigeni kumeandaa mwamko katika lugha na mila ya Gorwaa kwa kusema hivi, kuwa na timu ya watafiti wenyeji wa Gorwaa, na kuendeleza kazi hii kwa sehemu katika lugha yao binafsi na mila sambamba na muafaka na watafiti wan je itakuwa chimbuko kuu.

-Kwanza: Lugha na mila zitafaidi kutoka mtazamo wa ndani na mafanikio halisi kutokana na wenyeji.

-Pili: Watafiti wa nje watafaidi toka maendelezo ya kumbukumbu zilizowekwa kwa uwezo wa utafiti wa mradi mkubwa.

-Tatu: Ufanisi wa jamii kutokana na ustadi uliotoka kwenye watafiti kwenda kwa watu wengine binafsi. Kwa mfano elimu ya kompyuta, picha, ustadi wa mahojiano, kutaweza kufikirika, kutatiwa maanani.

Hatua hii ni ghali na ya gharama kubwa na muda mrefu ikihitaji kujitoa kwa hiari kutokana na watafiti wa nje na kufundisha stadi, na kwa watafiti wenyeji kuwa wenye busara, na walimu wenyewe.

Hatua hii itahusika na:

8A. Kutambua nafasi ya watafiti wenyeji katika agenda kwa utafiti wa Gorwaa(tazama hapo chini)

8B. Kutambua stadi inayohitajika.

8C. Kuendeleza, kujifunza ramani(mchoro) kuhakikisha watafiti wenyeji wanafundishwa stadi inayotakiwa.

8D. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

<u>Kuwasaidia watafsiri (wakalimani) wa lugha ya Kigorowa:</u>

Nchi ya Gorwaa mara zote ni ya makabila mengi kuna hatua fulani yenye lugha nyingi, ili kuhakikisha kuwa kazi katika lugha na mila ya Gorwaa haimwachi nje mtu yeyote, imeafikiwa kuwa watafsiri(wakalimani) kimsingi Gorwaa –Kiswahili wasaidiwe ili kutoa huduma kwa wasio tumia Gorwaa (wasiozungumzwa Kigorowa).

Hatua hii itahusika na:

9A.Kutambua lini na wapi watafsiri wa lugha ya Gorwaa malipo au watakavyofanya kazi.

9B. Kuandaa nafasi ya mafunzo kwa watafsiri wa Gorwaa (wakalimani).

9C. Kuhakikisha kuwa wasiozungumza Kigorowa wameandaliwa huduma za tafsiri katika matukio ya lugha ya Gorwaa.

9D. Kutathmini ufanisi wa lugha ya hatua hii.

<u>Kuendeleza agenda ya utafiti wa Gorwaa:</u>

Mengi ya hatua zilizoorodheshwa katika sehemu hii hazitaeleweka bila uelewa sahihi wa mawazo bunifu au maono makuu yaliyohusika(mbinu za siku hizi za kilimo, elimu rika ya utamaduni n.k.) Kwa haya ni muhimu kuwa agenda thabiti ya utafiti itambulishwe na kufuatwa na kamati.

Utafiti katika hali hii unatakiwa kuhusisha mambo mawili-utafiti wa kielimu-(ukifanywa na watu binafsi wahusikao na vyuo vikuu na vyuo vingine vya juu) na utafiti wa kujitolea bure usio na kipato(unaofanywa na watu wenyeji waliofundishwa).

Hatua hii itahusika na:

10A. Kutambulishwa ndani ya hatua maalumu pendekezwa kwa 2017-2022: Mawazo makuu muhimu kama funguo ambazo lazima zieleweke kabla ya kuchukua hatua.

10B. Kutoka hatua hizi kutambulisha watu maalumu kuendesha utafiti huu.

10C. Kusimamia na kusaidia watu hawa binafsi kuongoza utafiti madhubuti kwa muda muafaka.

10D. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

Kuendeleza mpango wa kilimo na utamaduni:
Msaada wa kilimo cha utamaduni (uliofafanuliwa kijuu juu kama kilimo cha mtama, maharage, na kukaribisha matunda mengine, mbogamboga na nafaka ambazo inaweza kuchukua nafasi muhimu katika mlo na uchumi wa Gorwaa). Umetambulishwa kama njia fanisi ya kupiga vita matokeo hasi ya ukoloni mamboleo kwa kuongezea, ili kuwa na uboreshaji kulingana na hali ya hewa inafaa kuliko kutambulisha mazao tajwa (hasa mahindi), kupanda, kupalilia, kuvuna, na ulaji wa mazao asili yote yanafungamanishwa katika sikukuu na shughuli za Kigorowa kwa kutafuta msimamo wa kati kwa kati; kati ya mbinu za kilimo cha kisasa na zile zilizofanywa kitamaduni na watu wa Gorwaa. Shughuli zote(sikukuu za mavuno, matumizi ya madawa ya asili kuulia wadudu, ulaji kwenye sahani za asili(vyombo) n.k. ). Unaweza tena kufanyika kwa makini na thabiti.
Hatua hii itahusika na;

11A. Kuendesha utafiti kwa kuamua zoezi la msingi la mbinu za kilimo cha asili na mbinu za kisasa za kilimo kuunganishwa pamoja . Katika njia hii inayoheshimiwa na kujali matukio yaliyoanzishwa na Gorwaa pamoja na kuhakikisha msaada wa kilimo kizuri.

11B. Kuendeleza mpango wa miaka 5 ambao unaanza na eneo linalomilikiwa na kamati na kuwa tayari kufanyika kama "shamba darasa" kuchukuliwa kama sehemu kuu Ya mpango wa kilimo na wakulima wenyeji katika Gorwaa yote.

11C. Kutathmini ufanisi wa hatua hii.

**Ratiba ya mpango (mpango kazi)**

| MWAKA | ROBO | SHUGHULI(MATUKIO) | MATOKEO |
|---|---|---|---|
| 2017 | 1Jan-Machi | 10ABC.<br>-Kuendeleza agenda kwa utafiti wa Gorwaa<br>11A.-Utafiti zoezi la kilimo cha jaribio | |
| | 2Aprili-Juni | 10ABC<br>-Kuendeleza agenda Ya utafiti wa Gorwaa<br>11A.-Kuendeleza zoezi la kilimo cha jaribio | 10ABC.<br>Agenda kwa utafiti wa Gorwaa<br>11A.<br>Kuendeleza kilimo cha jaribio. |
| | 3Julai-Sept. | 11B Kuendeleza mpango wa miaka mitano<br>8AB. Kutambulisha kazi ya watafiti wenyeji na stadi zinazohitajika. | |
| | 4 Oktoba-Desemba | 8C Kuendeleza kusoma ramani. | 1A Taarifa ya maendeleo ya mwaka.<br>11B. Mpango wa miaka 5. |
| Mwaka 2018 | 1Jan-Machi | 4ABC. Maombi ya mila ya Gorwaa | 8C. Kusoma ramani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 2Aprili-Juni | 3A. Kutambulisha orodha ya sehemu za jamii. | 4ABC Maombi ya mila ya Gorwaa |
| | 3Julai - Septemba | 3B Kuendesha mikutano midogo midogo na wajumbe wa vikundi.<br>4E Tathmini. | |
| | 4Oktoba - Desemba | 3B Kuendesha mikutano midogo na wajumbe wa vikundi. | 1A. Taarifa ya mwaka.<br>3B. Ustadi wa kuelezea na kuimarisha matumizi ya Gorwaa.<br>4E. Tathmini |
| Mwaka 2019 | 1Jan-Machi | 3C. Kufanikisha hizi stadi binafsi.<br>6ABC. Kupanga onyesho la Gorwaa | |
| | 2Aprili-Juni | 3C. Kufanikisha hizi stadi binafsi.<br>6E. Kutathmini onyesho la Gorwaa. | |
| | 3Julai- Septemba | 3C. Kufanikisha hizi stadi binafsi.<br>6E. Kutathmini onyesho la Gorwaa. | 6D. Kunakili mahudhurio, kupiga picha ya maonyesho ya Gorwa. |
| | 4Oktoba - Desemba | 3C. Kufanikisha hizi stadi binafsi.<br>6D. Kupanga onyesho la Gorwa. | 1A. Taarifa ya maendeleo ya mwaka. |
| MWAKA 2020 | 1Jan-Machi | 9A. Watafsiri wa lugha ya Gorwaa | 6E Tathmini ya onyesho la Gorwaa. |
| | 2Aprili-Juni | 3D. Tahtmini<br>9D Mafunzo ya watafsiri | |
| | 3Julai- Septemba | 3D. Tathmini<br>9D Mafunzo ya watafsiri | 3D. Tathmini |
| | 4Oktoba - Desemba | 10 D. Tathmini | 1A Taarifa ya miaka 4<br>1A. Taarifa ya maendeleo ya mwaka<br>8D. Tathmini<br>9C. Maandalizi ya watathmini |
| Mwaka 2021 | 1Jan-Machi | 1B. Anza hatua za mpango wa 2022-2027<br>7ABC. Kunakili nyimbo(kurekodi nyimbo 12)<br>C. Tathmini | 10D. Tathmini |
| | 2Aprili-Juni | 7D. Kurekodi nyimbo<br>9D. Tathmini | 11C. Tathmini |
| | 3Julai- Septemba | 7D. Kurekodi nyimbo<br>7E. Kuendeleza mpango wa usambazaji | 9D. Tathmini<br>7D.Kurekodi nyimbo za Gorwa |
| | 4Oktoba - Desemba | 7F. Kusambaza nyimbo | 1B. Hatua za mpango 2022-2027<br>1A. Taarifa ya maendeleo ya mwaka. |
| Mwaka 2022 | 1Jan-Machi | 7G. Tathmini | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 2Aprili-Juni | | 7G. Tathmini |
| | 3Julai-Septemba | | |
| | 4Oktoba -Desemba | | 1A. Taarifa ya maendeleo ya mwaka |

Hatua ya 2 na ya 5 ikitegemea kuwa na watafiti wa elimu ratiba itategemea zaidi ratiba ya mtafiti binafsi wa elimu.

Na Rev. Hezekiah H. Kodi

-------------------------------------

Mtafsiri